TANGAZO LA SERIKALI NA. la tarehe 26/10/2018

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA

(SURA. 290)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 6(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA MJI KIBAHA ZA MWAKA 2018

## SEHEMU YA KWANZA

## UTANGULIZI

Jina na tarehe ya kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Mji Kibahaza Mwaka 2018 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Mji Kibaha.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:-

"*Ada na* Ushuru" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri au wakala wake kwa ajili ya huduma, vibali, au leseni zitolewazo na Halmashauri;

"*Afisa Mwidhiniwa*" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa

Sheria Ndogo hizi;

"*Chombo cha Usafiri*" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha mtu, watu au mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine isipokuwa mkokoteni, au wanyama wanaotumika kama kusafirisha watu au mizigo;

"Gari" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha mtu, watu, mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine na chenye leseni ya kufanya shughuli hiyo;

"*Halmashauri*" maana yake ni Halmashauri ya Mji Kibaha;

"*Kibali cha Ujenzi*" maana yake ni kibali kinachotolewa na Halmashauri kwa ajili ya ujenzi ambao unafanyika ndani ya eneo la Mamlaka ya Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi au Kanuni na Sheria zinazosimamia ujenzi mjini ;

"Kizimba" maana yake ni meza, nafasi, sehemu nyingine katika soko inayotumika kwa ajili ya kuuzia bidhaa katika eneo la soko la Halmashauri;

"*Machinjio*" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi;

"*Maegesho*" maana yake ni sehemu yeyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha chombo cha usafiri kwa muda;

"*Masoko na gulio*" maana yake ni sehemu yoyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuuza na

kununua bidhaa;

"Matangazo" maana yake ni matangazo yanayotangazwa kwa kutumia vipaza sauti kwa ajili ya kutangaza biashara ya aina yoyote katika eneo la Halmashauri ikijumuisha matangazo ya masoko, magulio, sherehe, mikutano isipokuwa ya vifo na misiba;

"Mazao" maana yake ni mazao yote yatokanayo na shughuli za mashambani ikijumuisha na mazao ya chakula, biashara pamoja namazao ya misitu;

"Minara" maana yake ni minara yote itakayowekwa kwa ajili ya mawasiliano ya simu, fax, redio yenye urefu unaozidi mita ishirini (20) kutoka usawa wa ardhi;

"*Mhudumu*" maana yake ni mtu yeyote anayehudumia wateja katika eneo la biashara;

"*Mkurugenzi*" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kibahapamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"*Matangazo*" maana yake ni matangazo yanayotangazwa kwa kutumia vipaza sauti kwa ajili ya kutangaza biashara za aina yoyote katika eneo la Halmashauri ikijumuisha matangazo katika masoko, magulio, sherehe, mikutano isipokuwa matangazo ya vifo au misiba ;

"*Matangazo ya biashara*" maana yake ni matangazo yote ya sauti ambayo yanajumuisha Sanaa za maonyesho, Sanaa za ufundi, Muziki wa asili, Ususi, Michezo, Disko, Muziki wa dansi, Video,

Muziki wa taarabu, Maonyesho ya sinema, Mazingaombwe, fete na bahati nasibu, Tiba za jadi na matumizi ya viwanja vya michezo;

"*Usajili wa vyombo vya usafiri*" maana yake ni utaratibu utakaowekwa na Halmashauri wa kuorodhesha idadi ya vyombo vya usafiri vinavyofanya biashara ndani ya mamlaka ya Halmashauri;

"*Ushuru wa Soko*" maana yake ni ushuru ambao hutozwa kutokana na bidhaa zinazoletwa na kuuzwa sokoni ;

"*Wakala*" maana yake ni Mtu, Taasisi, Kampuni au Asasi yeyote iliyoteuliwa kisheria na Halmashauri kukusanya mapato kwa niaba ya Halmashauri ;

SEHEMU YA PILI :
NAMNA YA KUKUSANYA ADA NA USHURU

Ada na Ushuru

4. (1) Halmashauri itatoza Ada na Ushuru mbalimbali kwa ajili ya vibali, leseni na huduma zitolewazo na Halmashauri kama inavyoonyeshwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ada na Ushuru takaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kabla ya huduma kutolewa.

(3) Huduma zitakazotozwa Ada na Ushuru katika Sheria Ndogo hizi ni;-

a)Ada na vibali mbalimbali

b) Ada ya kukodi mali/vifaa vya halmashauri

c)Ada ya Upimaji afya ya Wahudumu

d) Ada ya Vibali vya ujenzi

e)Ada ya Ukaguzi wa nyama

f) Ushuru wa soko la wanyama

g) Kodi, ada na ushuru kwa matumizi ya masoko na magulio

h) Ushuru wa mazao

i) Ushuru wa maegesho

j) Ushuru wa maeneo yaliyosimikwa minara

k) Ada ya usajili wa vyombo vya biashara

l) Ushuru wa matangazo kwa kutumia vipaza sauti.

Wajibu wa kulipa Ada na Ushuru

5. (1) Itakuwa ni Wajibu wa kila Mtu anayetakiwa kulipa Ada na Ushuru kuhakikisha kwamba analipa kwa viwango vilivyoainishwa kwenye Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Muda wa kukusanya Ushuru utakuwa ni kuanzia Saa Kumi na mbili (12:00) kamili asubuhi mpaka saa kumi na mbili (12:00) kamili jioni.

(3) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo (2), Maafisa wa Halmashauri au Wakala anaweza kukusanya Ada na Ushuru baada ya muda uliotajwa hapo juu endapo atakuwa na kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri.

(4) Malipo ya Ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yeyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na

Mlipa Ada na Ushuru.

(5) Malipo ya Ushuru yanayotozwa kwa Mujibu wa Sheria Ndogo hizi yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi ya kieletroniki itakayothibitisha ulipaji wa malipo hayo.

Mabadiliko ya Viwango vya ada na ushuru

6. (1) Halmashauri itaweza kubadilisha viwango vya Ada na Ushuru pale itakapoona kuwa inafaa.

(2) Katika kufanya marekebisho ya viwango vya Ada na Ushuru au kipengele chochote katika Sheria Ndogo hizi, Halmashauri itafuata taratibu zote za utungaji wa Sheria Ndogo zinazoelekezwa na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura ya 288.

Uteuzi wa Wakala

7. Halmashauri inaweza kuteua Kampuni, Asasi au Taasisi yoyote kukusanya Ada na Ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika vyanzo vilivyokubaliwa kukusanywa na Wakala.

Wajibu wa Wakala

8. Wakala aliyeteuliwa chini ya Sheria Ndogo hizi atakuwa na wajibu wa-

(a) kukusanya na kupokea Ushuru katika eneo na Chanzo alichopangiwa kwa viwango vilichoainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi;

(b) kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya Mkataba wa Uwakala kati yake na Halmashauri;

Ukusanyaji wa Madeni

9. (1) Halmashauri inaweza kukusanya Ada na Ushuru kwa njia ya Mahakama endapo mtu au taasisi itakuwa imeshindwa kulipa Ada na Ushuru kwa muda uliokubaliwa.

(2) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika kifungu cha 1 hapo juu, Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya Ada au Ushuru kwa njia ya kukamata au kushikilia mali zinazohamishika za Wadaiwa zenye thamani sawa na deni la ada au ushuru pamoja na gharama za kukamata.

(3) Baada ya kipindi cha siku thelathini (30) kupita tangu kukamatwa kwa mali za Mdaiwa, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuziuza kwa njia ya mnada baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(4) Endapo mali zilizokamatwa zinaweza kuharibika kwa haraka, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuziuza kabla hazijaharibika baada ya kupata Idhini ya Mahakama.

(5) Bila kuathiri Masharti yaliyowekwa katika Kifungu Kidogo cha (3) na (4), Halmashauri kabla ya kuuza mali yoyote iliyokamatwa, Mkurugenzi atatoa taarifa ya siku saba kwa Mdaiwa na umma juu ya kusudio la kuuza mali hizo.

(6) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote ile itakayotokea ama wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri, isipokuwa kama hasara hiyo itakua imesababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri.

Ukaguzi

10. Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa :-

(a) kuingia katika jengo lolote kwa lengo la kukusanya ada na ushuru;

(b) kukagua eneo au chombo chochote atakachokitilia mashaka kuwa kinahifadhi au kusafirisha bidhaa au kinatumika kukwepa kulipa ada na ushuru.

SEHEMU YA III

MAKOSA NA ADHABU

Makosa

11. Itakuwa ni kosa Chini ya Sheria Ndogo hizi;

A. Kwa Wakala;

(a) atakusanya Ada na Ushuru bila kibali cha maandishi au mkataba toka kwa Halmashauri;

(b) atajaribu au atakusanya ada na ushuru kwa kiwango tofauti na kilichotajwa kwenye Sheria Ndogo hizi;

(c) atashindwa kuwasilisha au atawasilisha pungufu ya kiwango cha Ada na Ushuru alichokubaliwa katika mkataba;

(d) atakusanya Ada na Ushuru kwa mbinu tofauti na alizoelekezwa na Halmashauri

B. Kwa mtu yeyote ikiwa;

(a) atashindwa, atadharau, au atakaidi au atakataa kulipa Ada na Ushuru au kutekeleza agizo lolote

alilopewa na Halmashauri kuhusiana na ulipaji wa Ada na Ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi;

(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa Ada na Ushuru;

(c) atatengeneza, atatayarisha, ataidhinisha utengenezaji, au atatunza nyaraka za uongo kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa Ada na Ushuru mbalimbali ndani ya Halmashauri;

(d) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri, au Atashindwa au kutoa taarifa zitakazohitajika na Halmashauri;

(e) atashindwa kuweka Kumbukumbu, vitabu, hesabu, au maelezo yoyote yatakayohitajika Halmashauri; na

(f) atamzuia Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(g) atajenga jengo lolote bila kibali cha ujenzi;

(h) atachinja mifugo bila kukaguliwa;

(i) atafanya matangazo bila kuwa na kibali na kulipa ada;

(j) ataendesha gari kwa madhumuni ya biashara bila usajili;

(k) ataegesha gari katika maeneo yasiyoruhusiwa;

Adhabu

13. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi milioni moja (1,000,000/=) au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili (12) na kisichozidi miaka miwili (2) au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

14. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi laki tano (500,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari yake mwenyewe kwa maandishi na kukubali kutekeleza wajibu wake pamoja na kulipa faini anayodaiwa kama ilivyoekelezwa katika jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

Tangazo la Serikali Na. 190 la tarehe 10/10/2008

15. Sheria Ndogo hizi zinafuta Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Mji Kibaha, 2008.

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetungwa chini ya Kifungu cha 4(1)*

(i) ADA NA VIBALI MBALIMBALI

| Na. | Aina ya Kibali | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Kibali cha kuweka uzio/fensi ya muda kwa ajili ya kufanya ujenzi ili kulinda usalama wa watu na mali. | -Ujazo mdogo ( low density) - 120,000/=<br>-Ujazo wa kati ( medium density) - 75,000/=<br>-Ujazo mkubwa ( high density) - 30,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 2. | Kibali cha mabadiliko ya matumizi ya ardhi. | -Makazi kuwa biashara- 100,000/=<br>-Biashara kuwa Viwanda-200,000/=<br>-Makazi/Biashara kuwa kituo cha mafuta-200,000/=<br>-Shamba kuwa viwanja: - Ekari 1-5 shilingi 200,000/=<br>na ekari 5 na kuendelea shilingi 500,000/= |
| 3. | Kibali cha kukata/kufunga barabara za Halmashuri. | -Barabara ya lami shilingi – 200,000/=<br>- Barabara ya Vumbi shilingi- 100,000/=<br>- Barabara za changarawe- 150,000/= |
| 4. | Kibali cha kupitisha gari lenye mzigo zaidi ya tani kumi katika barabara za Halmashauri. | Shilingi milioni mbili (2,000,000/=) |
| 5. | Tozo ya thamani ya kupeana au mauzo ya kiwanja wakati wa umilikishwajiisipokuwa maeneo ya Serikali. | Asilimia tatu (3%) ya thamani ya kiwanja husika. |
| 6. | Kibali cha kufanya matangazo ya biashara maeneo mengine nje na minada, masoko na magulio. | Kwa siku shilingi 50,000/= |
| 7. | Ada ya usimikaji bango la biashara katika barabara za Halmashauri. | Shilingi 50,000/= kwa kila bango |

| | | |
|---|---|---|
| 8. | Ada ya maombi ya usajili wa Vyombo vya usafiri. | Shilingi 2000/= kwa kila fomu ya maombi |
| 9. | Kibali cha mazishi (maeneo ya kuzikia yanayomilikiwa na Serikali) | Shilingi 10,000/= kwa kimoja |
| 10. | Kibali kwa ajili ya shughuli za kiutamaduni | Ngoma na shughuli nyingine za kiutamaduni-10,000/=<br><br>Matamasha na sherehe nyingine – 20,000/= |

(ii)ADA YA KUKODI MALI/VIFAA VYA HALMASHAURI

| Na. | Aina ya Kifaa | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Ukumbi mkubwa wa Halmashauri | Si chini ya shilingi 200,000/= kwa siku |
| 2. | Ukumbi mdogo wa Halmashauri. | Si chini ya shilingi 150,000/= kwa siku |
| 3. | Lori la taka | Shilingi 25,000/= kwa tripu moja |
| 4. | Greda la Halmashauri | Si chini ya shilingi 700,000/= kwa masaa nane kwa siku |

(iii) ADA YA UPIMAJI AFYA

| Na. | Aina ya Ada | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Upimaji afya | Shilingi 10,000/= |

A: VIBALI VYA UJENZI

| Na. | Ukubwa wa eneo | Kiwango cha Tozo |
|---|---|---|
| 1. | $46.5m^2$ | 30,000/= |
| 2. | $46.5m^2$ hadi $92.01m^2$ | 36,000/= |
| 3. | $92.01m^2$ hadi $139.35m^2$ | 45,000/= |
| 4. | $139.35m^2$ hadi $185.81m^2$ | 60,000/= |
| 5. | $185.81m^2$ hadi $278.71m^2$ | 90,000/= |
| 6. | $278.71m^2$ hadi $371.61m^2$ | 150,000/= |
| 7. | $371.61m^2$ hadi $464.51m^2$ | 180,000/= |
| 8. | $464.51m^2$ hadi $557.42m^2$ | 210,000/= |

B: KIBALI CHA KUJENGA UZIO WA KUDUMU

| Na. | Ukubwa wa eneo | Kiwango cha Tozo |
|---|---|---|
| 1. | $100m^2$ hadi $600m^2$ | 45,000/= |
| 2. | $601m^2$ hadi $1600m^2$ | 75,000/= |
| 3. | $1601m^2$ hadi $4000m^2$ | 150,000/= |
| 4. | $4001m^2$ hadi $6000m^2$ | 300,000/= |
| 5. | Zaidi ya $6001m^2$ | 450,000/= |

C: KIBALI CHA KUJENGA MINARA (INSTALLATION CHARGES)

| Na. | Idadi | Kiwango cha Tozo |
|---|---|---|
| 1. | Kila mnara mmoja | 150,000/= kwa kibali |

(iv) ADA YA UKAGUZI WA NYAMA

| Na. | Aina ya Mnyama | Kiwango cha Tozo | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe/Punda | 2000/= | Kwa kila Ng'ombe |
| 2. | Mbuzi/Kondoo | 1000/= | Kwa kila Mbuzi/Kondoo |
| 3. | Mnyama mwingine yeyote | 1500/= | Kwa kila atakayechinjwa |

(v) USHURU WA SOKO LA WANYAMA NA NDEGE

| Na. | Aina ya Mnyama | Kiwango cha Tozo | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe/Punda | 2000/= | Kwa kila Ng'ombe/Punda kwa siku |
| 2. | Mbuzi/Kondoo | 1500/= | Kwa kila Mbuzi/Kondoo kwa siku |
| 3. | Mnyama mwingine yeyote | 1500/= | Kwa kila mnyama kwa siku |
| 4. | Kuku, bata na wengine wanaofanana na hao | 200/= | Kwa kila atakayechinjwa |

(vi) KODI, USHURU NA ADA KWA MATUMIZI YA MASOKO NA MAGULIO NA MAENEO MENGINE

| Na. | Aina ya biashara | Kiwango cha Tozo | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Kodi ya pango ya chumba/fremu | Si chini ya shilingi 8000m$^2$ kwa mwezi. | Kwa mita moja ya mraba |
| 2. | Ushuru wa soko, magulio na minada | 500/= | Kwa siku |
| 3. | Ushuru wa kuuza chakula mama lishe na baba lishe | 15000/= | Kwa mwezi |
| 4. | Ushuru wa tenga la nyanya, hoho, pilipili, bilinganya, bamia, nyanya chungu, karoti, matunda na vingine vinavyofanana na hivyo. | 500/= | Kwa kila tenga |
| 5. | Ushuru wa mkungu wa ndizi | 500/= | Kwa kila mkungu |
| 6. | Ushuru wa magunia ya nafaka yanayoshushwa ndani ya soko i.e mahindi, mchele, kunde, choroko, maharage, mbaazi na mazao mengine nje ya nafaka. | 2000/= | Kwa kila gunia lenye ujazo wa kilo mia moja. |
| 7. | Ushuru wa kufanya matangazo ya biashara kwa kutumia vipaza sauti katika masoko, magulio na minada | 10,000/= | Kwa siku |
| 8. | Ushuru wa vizimba | 15,000/= | Kwa mwezi |
| 9. | Ushuru wa choo | Haja ndogo na kubwa – 300<br>Huduma ya kuoga - | Kwa kila inapohitajika huduma |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | 500 | |
| 10. | Ushuru wa meza ndani ya soko | 500 | Kwa siku |

(vii) USHURU WA MAZAO

| Na. | Aina ya mazao | Kiwango cha ada |
|---|---|---|
| 1. | Mazao ya biashara | 3% ya bei ya kununulia |
| 2. | Mazao ya chakula | 2% ya bei ya kununulia |
| 3. | Mazao ya misitu | 3% ya bei ya kununulia |

(viii) USHURU WA MAEGESHO

| Na. | Muda wa uegeshaji | Kiwango cha ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Nusu saa | Shilingi 300/= |
| 2. | Saa moja | Shilingi 600/= |
| 3. | Siku nzima | Shilingi 1000/= |
| | | |

(ix) ADA YA USAJILI WA VYOMBO VYA USAFIRI

| Na. | Aina ya chombo | Kiwango cha ada |
|---|---|---|
| 1. | Taxi/kirikuu | 30,000/= kwa mwaka |
| 2. | Gari chini ya tani 7 | 40,000/= kwa mwaka |

| | | |
|---|---|---|
| 3. | Gari zaidi ya tani 7 | 50,000/= kwa mwaka |
| 4. | Bajaji/ toyo ( pikipiki matairi mitatu ) | 30,000/= kwa mwaka |
| 5. | Pikipiki ( tairi mbili ) | 20,000/= kwa mwaka |

JEDWALI LA PILI
HATI YA KUKIRI KOSA
(*Chini ya Kifungu cha 14*)

Mimi.......................................................................................................
...... nakiri mbele ya ........................................................... ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kibaha, kwamba, mnamo tarehe ....... ya mwezi ......... mwaka ............ nilitenda kosa la kukiuka masharti ya Kifungu cha ............ cha Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Mji Kibaha za mwaka 2018.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kibaha, kwa hiyari yangu niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru unaodaiwa pamoja na faini.

Nathibitisha maelezo hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu na ufahamu wangu.

Leo tarehe ...... ya mwezi ............... mwaka ............
Jina..........................................................................
Saini...............

Mbele ya:
Jina..........................................................
Cheo ........................................................
Saini ..........................................................

Lakiri ya Halmashauri ya Mji Kibaha imegongwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia Mkutano wa Baraza la Halmashauri ya Mji Kibaha uliofanyika tarehe 2/5/2018.

JENIFA C. OMOLO,
*Mkurugenzi*
*Halmashauri ya Mji*
*Kibaha*

L.S

LEONARD S. MLOWE,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya Mji*
*Kibaha*

NAKUBALI.

Dodoma,
4 Octoba, 2018

SELEMANI S.JAFO (MB.)
*Waziri wa Nchi-or Tamisemi*